

Jina..... Nambari yako...../.....
Shule..... Tarehe

102/2

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA 2

JUNI / JULAI - 2012

MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI WA PAMOJA WA WILAYA YA BUTERE- 2012
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari

102/2

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA 2

JUNI / JULAI - 2012

MUDA: SAA 2 ½

Maagizo

1. Andika jina lako na nambari yako katika nafasi iliyoachwa.
2. Weka sahihi yako na tarehe katika nafasi iliyoachwa
3. Jibu maswali yote
4. Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa

Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo.

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi — vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopsuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitishia hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung 'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwelesi zaidi ya kawaida. Hii husababisha na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kuitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahaba uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kingo zake wa kujinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujinga dhidi ya vidonda vya tomboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na ,ni rahisi kutokea tena baada ya kupora.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na Si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

MASWALI

- (a) Yape makala haya kichwa (alama 2)

- (b) Mbali na athari kwa uzazi wa kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. (alama 3)

- (c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara ~~kwa~~ wanawake hasa ni hatari mno. (alama 4)

visit www.freecsepa.org/pets

- (d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu (alamu 2)

Page 1 of 1 | Free KC

- (e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. (alam 3)

.....
.....
.....

- (f) Eleze maana ya msamiati ufuatao kama ulivyonumiwa kwenye taarifa.

(i) Gandwa

- (ii) Tunguka

.....

2. UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

RIPOTI YA SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE

Wakati wa kuzaliwa, kiwiliwili cha mtoto wa kike huwa kimekomaa vizuri zaidi kuliko cha wavulana aidha wao huwa na mfumo wa kinga ya kimwili bora kushinda wa watoto wa kiume.

Kwa sababu hii watoto wenye wa kiume huaga dunia kuliko wale wa kike kabla ya kutimiza miaka mitano. Kulingana na Benki ya Ulimwengu, takriban wavulana 112 kati ya 1000 huaga kabla ya kufikisha miaka mitano kinyume na wasichana 95 tu ambao huaga kabla ya kufikisha miaka mitano.

Hali hii ya watoto wa kike kuwa bora kuliko ya wale wa kiume hubadilika wanapofikia umri wa miaka 6. Uchunguzi wa kiuchumi unaonyesha kuwa mwaka 2010 takriban wavulana 736,700 walijiunga na darasa la kwanza huku wasichana 731,800 pekee wakijiunga na darasa la kwanza.

Kufikia mwisho wa darasa la 8, tofauti hii ilibainika zaidi ambapo asilimia 71 tu ya wasichana ndiyo iliyohitimisha elimu ya shule ya msingi ikilinganishwa na asilimia 74 ya wavulana hapa nchini Kenya.

Asilimia 43 pekee ya wasichana walijiunga na shule ya upili huku ile ya wavula na ikiwa 47. Asilimia 64 ya wasio na elimu nchini Kenya ni wasichana.

Si katika elimu tu ambapo wanawake hawajaimarika bali hata kiafya. Nchi ya Kenya bado ina visa vingi vya vifo vya wanawake wakati wa kujifungua duniani. Kwa kila wanawake 100,000 wanaojifungua nchini Kenya, wanawake 488 huaga dunia. Mwanamke nchini Kenya nafasi 1 kati ya 38 ya kuaga wakati wa kujifungua ikilinganishwa na 1 kati ya 1600 ya mwanamke nchini Mauritius.

Wanawake pia ni asilimia 58 ya watu waliokomaa ambao wanaishi na virusi vya ukimwi. Hata hivyo, wanawake bado wana uwezo mkubwa wa kuishi miaka mingi zaidi ya wanaume. Mwanamke anatarajiwa kuishi miaka 55 ikilinganishwa na miaka 54 ya wanaume.

Kuhusu maswala ya ndoa, mwanamke wa kiwango cha wastani huolewa akiwa na miaka 21.4 huku mwanamme akioa na miaka 26.2.

Umri wa kuolewa wa msichana huongezeka kiwango cha elimu kinapoongezeka, Uchunguzi uliofanywa hivi karibuni unaonyesha kuwa wasichana ambao hawajaelimika huolewa wakiwa na miaka 17.5 huku wale ambao wamesoma hadi kiwango cha shule ya upili wanaoleka wakiwa na umri wa miaka 22.4. Hii ni karibu miaka mitano baadaye.

Wanawake katika kiwango cha chini kabisa kiuchumi, huolewa wakiwa na miaka 18.6 kwa kuwa ndoa ndiyo njia rahisi sana ya kuwatoa katika hali ya umaskini pale wanapoolewa kwa wanaume tajiri. Kwa upande mwingine, mwanamke katika kiwango cha juu cha kichumi huolewa akiwa na umri wa miaka 22.6 yaani miaka minne baada ya wale wa kiwango cha chini kiuchumi.

Kwa wastani, mwanamke chini Kenya ana watoto 5.0 akiinganishwa na wale wa kizazi cha mamake ambao ni 7.2 na wa kizazi cha nyanyake ambao ni 7.5.

Wanawake na wanaume nchini Kenya wanatofautiana kwa kiasi kikubwa kwa idadi ya watoto wanaopata.

Wanaume wa mjini ambao wamehitimu elimu ya shule ya upili hupendelea kuwa na watoto 3.4 huku wale wa mashambani wakipendelea watoto 4.3. Kwa upande mwingine, wanawake ambao wana kisomo cha shule ya msingi wanaoishi mashambani hupendelea kupata watoto 4 ilhali wale wa mjini ambao wamehitimu kisomo cha shule ya upili hupendelea kupata watoto 3.

Kwa kuzingatia ~~kipato~~ wanaume matajiri nchini Kenya hupata watoto 3.4 huku wale maskini wakipata watoto 6.

Kwa wanawake assilia 20 ya wale matajiri hupata watoto 3 huku wale maskini wakipendelea kupata watoto 5.1

Nchi ya Kenya ina kiasi kikubwa cha wanawake wanaofanya kazi. Karibu 47 ya wafanyakazi ni wanawake. Hii ni idadi nzuri hasa kwa kuwa asilimia 50 ya watu nchini Kenya ni wanawake. Hata hivyo hali hii si ishara ya kupewa uwezo kwani wanawake wanahusishwa na kazi katika sekta zisizo rasmi, zisizokua na ambazo faida yake ni ya nchini sana kama vile; ushonaji, kuuza mboga na kuchuuza.

(Dondoo kutoka gazeti la Nation tarehe 8 machi ,2012 ,UK iv)

MASWALI

- (a) Wanawake na wanaume wanatofautiana kwa kiasi kikubwa.Kwa kurejereaa taarifa, thibitisha.(maneno 110-120) (alamu 9) (mtiririko 1)

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

(b) Kwa ithibati mwafaka tofauti kati ya wanawake.(maneno 50-60) (alamu 4) (utiririko 1)

NAKALA CHAFU

3. MATUMIZI YA LUGHA

- (a) Bainisha mfumo wa sauti katika neno lifuatalo (alama 2)

Masalkheri

- (b) Eleza matumizi manne ya kiimbo (alama 2)

- (c) Tambulisha viambishi katika neno lifuatalo (alama 4)

Nilichokutenganishia

(d) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali (alama 4)

Mwanafunzi aliyejata gredi ya A hakuwa mivivu shulenii

.....
.....
.....
.....

(e) Fuata maagizo (alama 2)

(i) Mgongwa amepewa dawa asubuhi(kauli ya kutendesheka mazoea)

.....
.....

(ii) Poa (Nafsi ya kwanza wingi, wakati ujao kauli ya kutendana.)

.....
.....

(f) Andika sentensi yakinishi kutokana na ifuatayo (alama 2)

Utarwala mbaya wa Bokono haukuzuilika

.....
.....

(g) Bainisha mwigiliano wa maneno katika sentensi ifuatayo (alama 3)

Walifunga ndoa juzi walakini ndoa yao ina walakini

.....
.....
.....
.....

(h) Tambua vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Mwanafunzi aliyesoma kwa bidii alipita mtihani

.....
.....

- (i) Tunga sentensi moja kubanisha matumizi ya vitate hivi (alama 2)

Ngoma

Goma

- (j) Bainisha maana ambili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Mwonyeshe atakayosoma.....

- (k) Tumia kitenzi kifuatacho kama kitenzi kisaidizi na kama kitenzi kishirikishi (alama 2)

Ndi-

- (l) Mwalimu huyu atawatahini wanafunzi wote watakaofanya mtihani (anza wanafunzi wote)(alama 2)

- (m) Jibu kulingana na maagizo kwenye mabano (alama 2)

(i) ujisadi (unda kitenzi)

(ii) -pya (unda nomino)

- (n) Tambua aina ya shamirisho katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Mama alimpikia chakula

(o) Andika sentensi zifuatazo kwa udogo (alama 2)

(i) Chungu changu kimevunjika

(ii) Ng'ombe wangu ana ndama mkubwa

(p) Kwa kutolea mifano, elezea matumizi matatu ya mshazari (alama 3)

(q) Kwa kuzingatia nafsi, tambua na uonyeshe mofimo katika sentensi ifuatayo (alama 2)

(i) Sisi tunampenda yeye tu.

(r) Tambua kirai kihuishi katika sentensi ifuatayo (alama 1)

Tulimkuta akiwa katika uchungu mwingi

4. ISIMU JAMII

Kuna madai kwamba lugha ya kiswahili ni zao la lugha za kibantu. Kwa mfano mitano thibitisha madai haya. *FreeEnglish* (alama 10)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com